TBARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2015

## 01 KISWAHILI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE MWAKA 2015

# KISWAHILI

Kimechapishwa na
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2016**

Haki zote zimehifadhiwa

## YALIYOMO


YALIYOMO ............................................................ iii

DIBAJI ............................................................ iv

1.0 UTANGULIZI ............................................................ 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI ............................................................ 1

2.1 Sehemu A: Imla ............................................................ 1
2.2 Sehemu B: Sarufi na Matumizi ya Lugha ............................................................ 5
2.3 Sehemu C: Lugha ya Kifasihi ............................................................ 11
2.4 Sehemu D: Ufahamu ............................................................ 25

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA MBALIMBALI ............................................................ 33

4.0 HITIMISHO ............................................................ 34

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ............................................................ 35

KIAMBATISHO CHA PEKEE ............................................................ 37

# DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa somo la Kiswahili imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wathibiti ubora wa elimu, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna wanafunzi walivyojibu maswali. Majibu ya wanafunzi katika upimaji ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo wanafunzi walijifunza kwa ufasaha na yale ambayo hawakujifunza katika kipindi cha miaka minne ya elimu ya msingi.

Katika taarifa hii, uchambuzi kwa kila swali umefanyika ambapo dosari mbalimbali zilizojitokeza wanafunzi walipokuwa wanajibu maswali zimeainishwa. Aidha, asilimia ya wanafunzi walioweza au kushindwa kujibu kwa usahihi imeoneshwa kwa kila swali. Uchambuzi umebaini kuwa baadhi ya wanafunzi walishindwa kujibu maswali kwa usahihi kutokana na mambo yafuatayo: kutokuwa na umahiri wa stadi za juu za kusoma na kuandika, kutofahamu kanuni za lugha na matumizi ya msamiati, kushindwa kutambua maelekezo ya swali na kuwa na uelewa mdogo wa mada mbalimbali katika somo.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho huu utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa lengo la kupata ufumbuzi wa dosari zilizoainishwa katika taarifa hii. Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania linaamini kuwa endapo maoni yaliyotolewa yatafanyiwa kazi ipasavyo, ujuzi na maarifa watakayopata wanafunzi yataongezeka na hatimaye ubora wa elimu na kiwango cha umahiri wa wanafunzi katika stadi mbalimbali kitaongezeka.

Mwisho Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani, Wataalamu wa TEHAMA na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii. Baraza litashukuru kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu kwa ujumla ambayo yatasaidia katika kuboresha taarifa ya uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa siku zijazo.



Dkt. Charles E. Msonde

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kuhusu namna ambavyo wanafunzi walijibu maswali ya upimaji wa somo la Kiswahili. Upimaji wa somo la Kiswahili ulikuwa na maswali **25** ambayo yaligawanywa katika sehemu nne ambazo ni: Sehemu A: *Imla*; B: *Sarufi na Matumizi ya Lugha*; C: *Lugha ya Kifasihi* na D: *Ufahamu*. Jumla ya wanafunzi **1,042,659** walisajiliwa kufanya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne ambapo miongoni mwao waliofanya upimaji wa somo la Kiswahili walikuwa **980,989** na kati yao wanafunzi **874,101** sawa na asilimia **89.1** walifaulu katika upimaji huo.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI

Sehemu hii inaainisha maswali yaliyoulizwa na majibu waliyoandika wanafunzi kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa kwa kila sehemu. Idadi na asilimia ya wanafunzi imeoneshwa kwa waliopata alama na waliopata sifuri kwa kila swali. Aidha, uchambuzi wa sababu zinazoweza kuwa zilichangia wanafunzi kushindwa kujibu maswali kwa usahihi au kujibu vizuri zimeainishwa. Rangi mbalimbali zimetumika kuonesha hali ya ufaulu, ambapo ufaulu kati ya asilimia 0 – 21 umewasilishwa kwa rangi nyekundu ikimaanisha ufaulu hafifu; 22 – 61 rangi ya njano ambao ni ufaulu wa wastani na 62 – 100 rangi ya kijani inayowakilisha ufaulu mzuri.

### 2.1 Sehemu A: Imla

Sehemu A ilikuwa na maswali matano ya Imla ambapo mwanafunzi alitakiwa kusikiliza kwa makini kila sentensi aliyosomewa kisha kuiandika kwa usahihi. Kila sentensi ilikuwa na maneno manne na kila neno lilikuwa na nusu alama, hivyo

kufanya kila sentensi sahihi kuwa na alama 2. Kwa ujumla sehemu hii ililenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika kusikiliza na kuandika sentensi zifuatazo:

**Swali la 1:** Dada atafua nguo zake.


**Swali la 2:** Bibi anasuka mkeka mpana.

**Swali la 3:** Baba ameleta matunda mengi.

**Swali la 4:** Baraka hucheza mpira jioni.

**Swali la 5:** Wananchi wengi walipiga kura.

Chati Na. 2.1.1 inaonesha asilimia za ufaulu katika sehemu A.




**Grafu 2.1.1**: Asilimia ya Wanafunzi Waliofaulu katika kila Swali

Maswali yote yalikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu ambapo wastani wa ufaulu ulikuwa asilimia 87.24. Swali la 1 ndilo lililojibiwa vizuri na idadi kubwa ya wanafunzi (asilimia 89.9) likifuatiwa na swali la 3 (asilimia 89.5), swali la 2 (asilimia 88.8), swali la 4 (asilimia 85.2) na swali la 5 (asilimia 82.8) kama

ilivyooneshwa kwenye grafu 2.1.1. Katika maswali yote wanafunzi waliopata alama zote 2 ni (asilimia 82.8). Kielelezo 2.1.1 kinaonesha majibu ya mmoja wa wanafunzi aliyezingatia taratibu za uandishi kama vile kuandika neno la kwanza kwa kila sentensi kwa kuanza na herufi kubwa pia kuweka nukta (.) mwishoni mwa sentensi zote tano kwa usahihi.

**Kielelezo 2.1.1**

Katika swali la 1 – 5, **sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

1. Dada atafua nguo zake.
2. Bibi anasuka mkeka mpana.
3. Baba ameleta matunda mengi.
4. Baraka hucheza mpira jioni.
5. Wananchi wengi walipiga kura.

Kielelezo 2.1.1 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeandika sentensi zote tano kwa usahihi.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wapo wanafunzi waliopata alama kati ya nusu na moja na susu kwa kuwa walikuwa na dosari mbalimbali za kiuandishi zilizosababishwa na mambo kama vile athari za lugha ya awali (lugha mama) kwa mfano, badala ya kuandika neno *Ba**r**aka* waliandika *Ba**l**aka*, *ku**l**a* badala ya *ku**r**a* na *mpi**l**a* badala ya *mpi**r**a*. Wanafunzi hao walishindwa kutofautisha sauti /r/ na /l/. Aidha, wapo walioandika neno ***ha**nafua* badala ya ***a**nafua* kwa kushindwa kutofautisha sauti /ha/ na /a /. Vilevile, baadhi ya wanafunzi walichanganya silabi huru na silabi mwambatano kwa kuandika neno *huche**nza*** badala ya *huche**za***; *walipi**nga***

badala ya *walipi**ga***; *matu**da*** badala ya *matu**nda*** na *me**gi*** badala ya *me**ngi***. Aidha, baadhi ya wanafunzi badala ya kuandika neno ***mwananchi*** waliandika **"*mwana*"** na **"*nchi*"** kama maneno mawili tofauti kwa sababu hawakuwa na umahiri katika uandishi wa maneno mwambatano. Kielelezo 2.1.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi mwenye dosari mbalimbali za kiuandishi.

**Kielelezo 2.1.2**

Katika swali la 1 – 5, **sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.


1. dada hata fuha ngwzake
2. Bibi hanasuka mkaka mpana
3. Baba hame leta matunga mengi
4. Baraka huchezampila hisiku
5. wana ndichi wengi wali piga kula

Kielelezo 2.1.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kutofautisha sauti /r/ na /l/, /a/ na /ha/, kuandika maneno mwambatano na kuacha nafasi kati ya neno na neno.

Aidha, asilimia 12.76 ya wanafunzi waliojibu maswali ya imla walipata alama 0. Wanafunzi hao walishindwa kutambua na kuandika maneno katika sentensi walizosomewa. Miongoni mwao wapo waliokuwa na uwezo wa kuandika herufi zinazowakilisha sauti mbalimbali lakini walishindwa kuunganisha herufi hizo kuunda silabi ili kupata maneno sahihi yanayounda sentensi. Kielelezo 2.1.3 ni sampuli ya majibu ya

mmoja wa wanafunzi aliyeshindwa kuandika sentensi hata moja kwa usahihi.

**Kielelezo 2.1.3**



Katika swali la 1 – 5, **sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.


Kielelezo 2.1.3 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kuunganisha herufi/silabi ili kupata maneno yanayounda sentensi alizosomewa.

## 2.2 Sehemu B: Sarufi na Matumizi ya Lugha

**Swali la 6:** Mama yangu __________________ chakula kizuri jana jioni.

A. anapika
B. atapika
C. alipika
D. hupika.

Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika matumizi ya njeo. Wanafunzi 776,694 (asilimia 79.2) waliweza kujibu swali hili vizuri kwa kuchagua chaguo sahihi C “alipika” kama ilivyooneshwa katika jedwali 2.2.1.




**Grafu 2.2.1:** Asilimia ya Wanafunzi kwa Kila Jibu

Wanafunzi hao walikuwa na uwezo wa kuhusisha neno jana na umbo -li- linalowakilisha njeo ya wakati uliopita.

Aidha, wanafunzi 204,295 sawa na asilimia 20.8 walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi kwani walichagua vipotoshi kati ya A "anapika," B "atapika," na D "hupika" ambayo siyo majibu sahihi. Vitenzi hivyo vina maumbo yanayowakillisha njeo ya wakati uliopo -na- katika neno anapika, ujao -ta- katika neno atapika, na umbo la hali ya mazoea -hu- katika neno hupika.

**Swali la 7:** Siku ya pili baada ya leo huitwaje?

A. Juzi
B. Kesho kutwa
C. Mtondogoo
D. Mtondo.

**Jedwali 2.2.1:** Idadi na Asilimia ya Wanafunzi katika kila Jibu

| Chaguo | Jibu Sahihi | Vipotoshi |
|---|---|---|
| **Idadi ya Wanafunzi** | 547,027 | 433,962 |
| **Asilimia ya Wanafunzi** | 55.8 | 44.2 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kutambua maneno yanayotaja siku tofauti baada ya leo. Jedwali 2.2.2 linaonesha kuwa wanafunzi 547,027 (asilimia 55.8) waliweza kujibu swali hili kwa usahihi kwa kuchagua jibu B "kesho kutwa."


Wanafunzi 433,962 (asilimia 44.2) walichagua vipotoshi kati ya A "juzi" neno lenye maana ya siku iliyotangulia jana, C "mtondogoo" neno lenye maana ya siku inayofuata mtondo yaani siku ya nne baada ya leo, na D "mtondo" lenye maana ya siku inayofuata keshokutwa, majibu hayo yote hayakuwa sahihi.

**Swali la 8:** Wingi wa neno ufundi ni upi kati ya maneno yafuatayo?

A. Mafundi
B. Fundi
C. Vifundi
D. Ufundi.

Swali hili lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika kutumia nomino za umoja na wingi. Wanafunzi 308,263 sawa na asilimia 31.4 walijibu swali hili vizuri kwa kuchagua chaguo D "ufundi" ambalo ndilo jibu sahihi kama ilivyooneshwa katika chati 2.2.3.

**Chati 2.2.1:** Asilimia ya Wanafunzi katika kila Jibu




Neno ufundi maana yake ni ujuzi au uwezo fulani wa kutenda jambo. Neno hili halina wingi kwa sababu ni nomino dhahania inayoonesha hali ya uwezo au ujuzi fulani.

Wanafunzi 672,726 (asilimia 68.6) walichagua kati ya vipotoshi A "mafundi" ambalo ni wingi wa neno "fundi" lililopo katika kipotoshi B lenye maana ya mtu mwenye ujuzi fulani na awezaye kufundisha wengine na kipotoshi C "vifundi" ni neno lililotokana na udogoishi/udunishi wa neno mafundi.

**Swali la 9:** Ni neno lipi kati ya maneno yafuatayo lenye maana inayojumuisha maneno; *upinde*, *bunduki*, *mkuki* na *mshale*?

A. Silaha


B. Vipuri

C. Malighafi

D. Samani.

Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kuhusu maneno yenye maana ya kimsamiati inayojumuishwa na neno moja. Katika swali hili mwanafunzi alitakiwa kuchagua neno moja linalojumuisha *upinde, bunduki, mkuki,* na *mshale*. Grafu 2.2.4 inaonesha kuwa wanafunzi 793,491 (asilimia 80.9) waliweza kujibu swali hili kwa usahihi kwa kuchagua chaguo A "silaha" ambapo katika muktadha wa kimatumizi *upinde, bunduki, mkuki, na mshale* ni vitu vinavyotumika kupigia au kupigania ambavyo vinaweza kujeruhi au kuua.

Wanafunzi 187,498 (asilimia 19.1) walichagua kati ya vipotoshi B "vipuri", C "malighafi" na D "samani" ambavyo maneno jumuishi ya *upinde, bunduki, mkuki*, na *mshale*. "Vipuri" ni neno jumuishi la vifaa vya kurekebisha mashine wakati "malighafi' ni neno jumuishi la mali za aina mbalimbali kwa ajili ya kuzalishia bidhaa za viwandani. "Samani" ni neno jumuishi la vifaa kama vile *viti, kabati, kitanda na meza*.




**Grafu 2.2.2:** Asilimia ya Wanafunzi katika kila Jibu

**Swali la 10:** Mwakani ____________________darasa la tano.

Ni neno lipi linakamilisha sentensi hiyo kwa usahihi?

A. niliingia
B. ninaingia
C. nitaingia
D. nimeingia

**Jedwali 2.2.2:** Idadi na Asilimia ya Wanafunzi katika kila Jibu

| Chaguo | Jibu Sahihi | Vipotoshi |
|---|---|---|
| **Idadi ya Wanafunzi** | 663,699 | 317,290 |
| **Asilimi ya Wanafunzi** | 67.7 | 32.3 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kuhusu njeo. Swali lilimtaka mwanafunzi kuchagua neno litakalokamilisha sentensi inayohitaji neno lenye mofimu ya njeo ya wakati ujao. Jedwali 2.2.5 linaonesha kuwa wanafunzi 663,699 (asilimia 67.7) walichagua chaguo C "nitaingia" ambalo ni jibu sahihi. Wanafunzi hao waliweza kubaini kuwepo kwa mofimu "ta" katika neno *ni**ta**ingia* inayowakilisha njeo ya wakati ujao ambayo inaendana na neno mwakani.

Wanafunzi 317,290 (asilimia 32.3) walichagua kipotoshi B "ninaingia" ambacho siyo jibu sahihi kwa sababu mofimu "na" inawalikisha njeo ya wakati uliopo ambayo haina upatanisho wa kisarufi na neno mwakani ambalo lipo mwanzoni mwa sentensi. Aidha, miongoni mwao walichagua kipotoshi A "niliingia" chenye mofimu "li" inayowakilisha njeo ya wakati uliopita na D

"nimeingia" chenye mofimu "me" inayowakilisha hali timilifu bila kuzingatia kuwa neno mwakani linaonesha kuwa jambo husika bado halijafanyika.

## 2.3 Sehemu C: Lugha ya Kifasihi

**Swali la 11:**___________________________si mkulima.

Swali lililenga kupima uelewa wa mwanafunzi kuhusu muundo wa methali ambapo mwanafunzi alitakiwa kuandika maneno yanayokamilisha methali husika. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na ufaulu mzuri kwani wanafunzi 654,963 (asilimia 66.8) waliandika "Mchagua jembe" ambacho kilikuwa kikamilisho sahihi cha methali husika. Wanafunzi hao waliweza kukamilisha methali husika kwa usahihi kwa sababu methali hii inatumiwa sana katika mawasiliano ya siku kwa siku miongoni mwa wanajamii wa hadhi zote. Kielelezo 2.3.1 kinaonesha jibu la mmoja wa wanafunzi aliyeandika jibu linalokamilisha methali husika kwa usahihi.

**Kielelezo 2.3.1**


11. Mchagua jembe si mkulima.

Kielelezo 2.3.1 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kukamillisha muundo wa methali kwa usahihi.


Aidha, wanafunzi 326,026 (asilimia 33.2) walipata alama 0 kama ilivyooneshwa katika jedwali 2.3.1.

**Jedwali 2.3.1:** Idadi na Asilimia ya Wanafunzi katika kila Alama

| Alama | 0 | 2 |
|---|---|---|
| **Idadi ya Wanafunzi** | 326,026 | 654,963 |
| **Asilimia ya Wanafunzi** | 33.2 | 66.8 |


Baadhi ya wanafunzi hao walishindwa kukamilisha methali husika kwa sababu hawakuwa na umahiri wa kuandika na wengine waliandika majibu ambayo vikamilisho vya muundo wa methali husika. Kielelezo 2.3.2 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kukamilisha kwa usahihi methali aliyoulizwa.

**Kielelezo 2.3.2**




Kielelezo 2.3.2 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika maneno ambayo si vikamilisho vya methali husika.


**Swali la 12:** Biashara ________________________.




**Grafu 2.3.1:** Asilimia ya Wanafunzi katika kila Alama

Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kukamilisha muundo wa methali ambapo mwanafunzi alitakiwa kuandika neno/maneno ili kukamilisha muundo wa methali husika kwa usahihi. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya na idadi kubwa ya wanafunzi. Grafu 2.3.2 inaonesha kuwa wanafunzi 836,881 (asilimia 85.3) walipata alama 0 kwa kuwa waliandika maneno ambayo katika muktadha wa kawaida yanahusiana na neno biashara lakini si vikamilisho vinavyounda methali husika. Baadhi ya maneno waliyoandika ni kama vile: *haimtupi muuzaji, haikosi wateja, huleta faida, huniletea faida nyingi, kupata faida, inalipa, ni uchumi, pamba na tumbaku, si biashara, hupatia ajira, haiishi,* na *imani*. Kielelezo 2.3.3 kinaonesha jibu la wanafunzi aliyeandika mambo mengine yahusuyo biashara lakini si kikamilisho cha methali husika.

**Kielelezo 2.3.3**


12. Biashara inalipa.

Kielelezo 2.3.3 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika faida ya biashara badala ya kukamilisha methali.

Aidha, wanafunzi 144,108 (asilimia 14.7) kama ilivyooneshwa katika grafu 2.3.2 waliweza kukamilisha methali husika kwa kuandika neno “haigombi” ambalo ni jibu sahihi. Biashara hutegemea makubaliano hivyo hakuna haja ya kugombana. Kielelezo 2.3.4 kinaonesha jibu la mmoja wa wanafunzi aliyeweza kukamilisha methali kwa usahihi.

**Kielelezo 2.3.4**

12. Biashara______________hangumbi______________.

Kielelezo 2.3.4 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyebaini muktadha wa matumizi ya neno biashara hivyo kuandika jibu sahihi.

**Swali la 13:**_________________ huumiza matumbo.

**Jedwali 2.3.2:** Idadi na Asilimia ya Wanafunzi katika kila Alama

| Alama | 0 | 2 |
|---|---|---|
| **Idadi ya Wanafunzi** | 641,855 | 339,134 |
| **Asilimia ya Wanafunzi** | 65.5 | 34.5 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kukamilisha muundo wa methali ambapo mwanafunzi alitakiwa kuandika neno linalokamilisha sehemu ya methali husika kwa usahihi. Jedwali 2.3.3 linaonesha kuwa wanafunzi 641,855 (asilimia 65.4) waliweza kukamilisha methali husika kwa kuandika neno sahihi "ngojangoja". Methali hiyo hutumika mara kwa mara katika miktadha mingi ya mawasiliano ya jamii katika kuhimiza watu kutenda mambo kwa wakati ufaao. Matumizi hayo yaliwafanya wanafunzi hao kukamilisha muundo wa methali kwa usahihi. Kielelezo 2.3.5 kinaonesha mmoja wa wanafunzi aliyeandika jibu sahihi.


**Kielelezo 2.3.5**

13. Ngojangoja______________huumiza matumbo.

Kielelezo 2.3.5 ni sampuli ya jibu sahihi la mwanafunzi

Aidha, wanafunzi 339,134 sawa na asilimia 34.6 waliandika maneno ambayo hayakamilishi methali husika kwa usahihi na miongoni mwao walishindwa kukamilisha muundo wa methali husika kwa sababu hawakuwa na stadi ya kuandika na hivyo kuandika herufi zisizokuwa na maana kisarufi. Kielelezo 2.3.6 kinaonesha jibu la mmoja wa wanafunzi aliyeshindwa kukamilisha methali husika.


**Kielelezo 2.3.6**




Kielelezo 2.3.6 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kuandika kikamilisho sahihi cha methali aliyopewa.

**Swali la 14:** Mpiga ngumi ukuta ___________________.

**Chati 2.3.1:** Asilimia ya Wanafunzi katika kila Alama



Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kukamilisha muundo wa methali. Mwanafunzi alitakiwa kuandika maneno ili kukamilisha muundo wa methali husika kwa usahihi. Chati 2.3.4 inaonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa wa chini sana ambapo wanafunzi 877,691 (asilimia 89.5) walishindwa kukamilisha methali husika kwa usahihi. Baadhi ya wanafunzi hao waliandika maneno kama vile "*huumia mwenyewe", "litakugeukia mwenyewe" "bondia",* na *"baunsa"* ambayo vikamilisho vya muundo wa methali husika. Wanafunzi walioandika "bondia" walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Wanafunzi hao waliandika jina la mtu anayecheza mchezo wa ngumi na "baunsa" ambalo si neno rasmi la kiswahili linalompambanua mtu mwenye nguvu aghalabu kutokana na mazoezi yakiwemo ya ngumi. Kielelezo 2.3.7 kinaonesha jibu la mmoja wa wanafunzi aliyeshindwa kuelewa matakwa ya swali.

**Kielelezo 2.3.7**

14. Mpiga ngumi ukuta___bondia___.

Kielelezo 2.3.7 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika jina la jumla la mtu anayecheza mchezo wa ngumi badala ya kukamilisha methali.

Aidha, wanafunzi 103,298 (asilimia 10.5) waliandika maneno "huumiza mkonowe" ambayo yanakamilisha muundo wa methali husika kwa usahihi. Wanafunzi hao walionesha kufahamu uhusiano wa mkono na kupiga ukuta ngumi kwani kwa kupiga ukuta ni dhahiri kuwa kitakachoumia ni mkono na si sehemu nyingine ya mwili au ukuta. Kielelezo 2.3.8 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyekuwa na umahiri katika methali husika.

**Kielelezo 2.3.8**

14. Mpiga ngumi ukuta huumiza mkonowe.

Kielelezo 2.3.8 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika kikamilisho sahihi cha methali husika.

**Swali la 15:** Dau la mnyonge ____________________.

**Jedwali 2.3.3:** Idadi na Asilimia ya Wanafunzi katika kila Alama

| Alama | 0 | 2 |
|---|---|---|
| **Idadi ya Wanafunzi** | 605,264 | 375,725 |
| **Asilimia ya Wanafunzi** | 61.7 | 38.3 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kukamilisha muundo wa methali. Swali lilimtaka mwanafunzi kuandika maneno yanayokamilisha muundo wa methali husika kwa usahihi. Jedwali 2.3.5 linaonesha kuwa wanafunzi wengi (asilimia 61.7) walishindwa kukamilisha methali husika kwa kuandika maneno ambayo siyo vikamilisho vya methali husika kama ilivyooneshwa kwenye kielelezo 2.3.9.

**Kielelezo 2.3.9**

15. Dau la mnyonge ipo siku litakwisha.

Kielelezo 2.3.9 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika maneno ambayo siyo kikamilisho cha methali husika.

Wanafunzi 375,725 (asilimia 38.3) walikamilisha methali kwa kuandika maneno sahihi “haliendi joshi”. Msemo “kwenda joshi” maana yake ni kwenda kasi, hivyo haliendi joshi maana yake ni

kwenda kwa mwendo mdogo au kukosa msukumo. Wanafunzi hao waliweza kukamilisha methali husika kwa sababu hii ni miongoni mwa methali zitumikazo katika jamii kuonesha kuwa maombi (dua) atoayo mtu wa hadhi ya chini (mnyonge) hayakamilishwi kwa wakati muafaka. Kielelezo 2.3.10 ni sampuli ya jibu la mmoja wa wanafunzi aliyekamilisha methali husika kwa usahihi.

**Kielelezo 2.3.10**

15. Dau la mnyonge ______haliendi joshi______.

Kielelezo 2.3.10 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyeandika kikamilisho sahihi cha methali husika.

Katika **swali la 16 hadi 20**, mwanafunzi alitakiwa kuandika maana ya nahau na kutegua vitendawili kwa kuchagua neno/maneno sahihi kutoka katika kisanduku kifuatacho:

| |
|---|
| tausi, kumpongeza, yai, chakula, moto, kutoa rushwa, mpira, kinyonga, kulipa kodi |

**Swali la 16:** Nahau "kumpa heko "maana yake ni ipi? ___________________.

**Jedwali 2.3.4:** Idadi na Asilimia ya Wanafunzi katika kila Alama

| Alama | 0 | 2 |
|---|---|---|
| **Idadi ya Wanafunzi** | 384,096 | 596,893 |
| **Asilimia ya Wanafunzi** | 39.2 | 60.8 |

Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi kuhusu maana ya nahau kwa kuchagua neno lenye maana sahihi ya nahau aliyopewa. Wanafunzi 596,893 (asilimia 60.8) walipata alama zote 2 kama ilivyooneshwa katika jedwali 2.3.6 wanafunzi hao walichagua maana sahihi ya nahau husika ambayo ni “kumpongeza”. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa maana ya neno “heko” ambayo ni shangilio la kumpongeza mtu. Kielelezo 2.3.11 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika neno lenye maana sahihi ya nahau.

**Kielelezo 2.3.11**

16. Nahau “kumpa heko” maana yake ni ipi? Kumpongeza

Kielelezo 2.3.11 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika maana sahihi ya nahau husika.

Aidha, wanafunzi 384,096 (asilimia 39.2) walichagua maneno ambayo hayana maana sahihi ya nahau husika. Wanafunzi hao hawakuwa na uelewa wa maana ya nahau hiyo jambo lililowafanya waandike maneno kama vile *chakula*, *moto* na *kutoa* kama inavyoonekana kwenye kielelezo 2.3.12 cha jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kubaini maana sahihi ya nahau husika.

**Kielelezo 2.3.12**

16. Nahau “kumpa heko” maana yake ni ipi? kutoa

Kielelezo 2.3.12 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika neno ambalo halisadifu maana ya nahau husika.

**Swali la 17:** Kitendawili kisemacho “tajiri wa rangi” jibu lake ni lipi?_______________.

**Jedwali 2.3.5:** Idadi na Asilimia ya Wanafunzi katika kila Alama

| **Alama** | **0** | **2** |
|---|---|---|
| **Idadi ya Wanafunzi** | 202,204 | 778,785 |
| **Asilimia ya Wanafunzi** | 20.6 | 79.4 |

Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi wa kutegua kitendawili kwa kuchagua jibu sahihi kati ya maneno aliyopewa kwenye kisanduku. Jedwali 2.3.7 linaonesha kuwa wanafunzi 778,785 (asilimia 79.4) walipata alama zote 2 kwani waliandika neno “kinyonga” ambalo lilikuwa jibu sahihi. Kinyonga hubadili rangi ya mwili wake ili ifanane na rangi ya mazingira aliyomo kama tahadhari kwa usalama wake. Ndiyo maana anaonekana ana utajiri wa rangi. Kielelezo 2.4.1 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 2.3.13**

17. Kitendawili kisemacho “tajiri wa rangi” jibu lake ni lipi? Kinyonga

Kielelezo 2.3.13 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyetegua kitendawili.

Aidha, wanafunzi 202,204 (asilimia 20.6) walipata alama 0 kwa sababu waliandika maneno ambayo hayategui kitendawili husika. Wanafunzi hao walishindwa kuhusisha utajiri wa rangi na sifa za kinyonga na hivyo kuchagua maneno ambayo hayakutegai kitendawili walichopewa. Kielelezo 2.3.14 ni sampuli ya jibu la mmoja wa wanafunzi aliyeandika neno ambalo halikutegua kitendawili alichoulizwa.

**Kielelezo 2.3.14**

17. Kitendawili kisemacho "tajiri wa rangi" jibu lake ni lipi? kumpongeza

Kielelezo 2.3.14 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kuhusianisha utajiri wa rangi na tabia ya kinyonga.

**Swali la 18:** Nahau "kuzunguka mbuyu" maana yake ni ipi?______________.

**Jedwali 2.3.6:** Idadi na Asilimia ya Wanafunzi katika kila Alama

| Alama | 0 | 2 |
|---|---|---|
| **Idadi ya Wanafunzi** | 487,860 | 493,129 |
| **Asilimia ya Wanafunzi** | 49.7 | 50.3 |

Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi wa kuchagua maana sahihi ya "kuzunguka mbuyu" kati ya maneno aliyopewa kwenye kisanduku. Takwimu katika jedwali 2.3.8 zinaonesha kuwa swali hili ni miongoni mwa maswali ambayo yamejibiwa kwa kiwango cha wastani. Wanafunzi 493,129 (asilimia 50.3) walipata alama zote 2 kwani walichagua maana sahihi ya nahau husika ambayo ni "kutoa rushwa". Kielelezo 2.3.15 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyeandika neno lenye maana sahihi ya nahau husika.

**Kielelezo 2.3.15**

18. Nahau "kuzunguka mbuyu" maana yake ni ipi? Kutoa rushwa

Kielelezo 2.3.15 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyeandika maana sahihi ya nahau aliyoulizwa.

Wanafunzi 487,860 (asilimia 49.7) walipata alama 0 kwa sababu waliandika machaguo ambayo hayaelezi maana sahihi ya nahau husika. Wanafunzi hao walishindwa kuhusisha tendo

la “kuzunguka mbuyu,” mti wenye shina nene kuliko miti mingine ambao unaweza kusababisha kuwa katika hali ya kutoonekana kama ilivyo katika tendo la kutoa rushwa ambalo pia hufanyika kwa kificho. Kielelezo 2.3.16 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kuhusianisha tendo la kutoa rushwa na “kuzunguka mbuyu.”

**Kielelezo 2.3.16**

18. Nahau “kuzunguka mbuyu” maana yake ni ipi? mlika

Kielelezo 2.3.16 ni sampuli ya jibu la mwanfunzi aliyeandika neno ambalo si maana ya nahau husika

**Swali la 19:** Kitendawili kisemacho “rafiki yangu ni mharibifu lakini bado ninamhitaji” jibu lake ni lipi? ______________

**Jedwali 2.3.7:** Idadi na Asilimia ya Wanafunzi katika kila Alama

| Alama | 0 | 2 |
|---|---|---|
| **Idadi ya Wanafunzi** | 288,068 | 692,921 |
| **Asilimia ya Wanafunzi** | 29.4 | 70.6 |

Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi kutegua kitendawili kwa kuchagua jibu sahihi kati ya maneno aliyopewa kwenye kisanduku. Jedwali 2.3.9 linaonesha kuwa wanafunzi 692,921 (asilimia 70.6) walipata alama zote 02 kwani waliandika neno “moto” ambalo lilikuwa jibu sahihi. Wanafunzi hao walichagua jibu “moto” kwa sababu moto unaweza kuunguza vitu lakini pia unahitajika kuwezesha shughuli mbalimbali muhimu kama kupika na kupasha joto. Kielelezo 2.3.17 kinaonesha jibu la

mwanafunzi aliyebaini na kuandika neno ambalo linaweza kuwa na sifa ya uharibifu na urafiki.

**Kielelezo 2.3.17**

19. Kitendawili kisemacho "rafiki yangu ni mharibifu lakini bado ninamhitaji" jibu lake ni lipi? moto

Kielelezo 2.3.17 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyetegua kitendawili.

Aidha, wanafunzi 288,068 (asilimia 29.4) walipata alama 0 kwa sababu waliandika maneno ambayo hayategui kitendawili husika. Wanafunzi hao walishindwa kubaini kwamba moto ni neno ambalo lina hadhi ya urafiki na uharibifu ikilinganishwa na maneno mengine waliyopewa kwenye kisanduku. Kielelezo 2.3.18 ni jibu la mmoja wa wanafunzi aliyeshindwa kutegua kitendawili husika.

**Kielelezo 2.3.18**

19. Kitendawili kisemacho "rafiki yangu ni mharibifu lakini bado ninamhitaji" jibu lake ni lipi? kinyonga

Kielelezo 2.3.18 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kubaini kuwa moto unaweza kuleta uharibifu lakini unahitajika.


**Swali la 20:** Nyumba yangu haina mlango" Jibu la kitendawili hiki ni _____________.

**Jedwali 2.3.8:** Idadi na Asilimia ya Wanafunzi katika kila Alama

| Alama | 0 | 2 |
|---|---|---|
| **Idadi ya Wanafunzi** | 199,492 | 781,497 |
| **Asilimia ya Wanafunzi** | 20.3 | 79.7 |

Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi wa kutegua kitendawili kwa kuchagua jibu sahihi kati ya maneno aliyopewa kwenye kisanduku. Wanafunzi 781,497 (asilimia 79.7) kama ilivyooneshwa katika jedwali 2.3.10 walipata alama zote 2 kwani waliandika neno "yai" ambalo lilikuwa jibu sahihi. Wanafunzi hao waliweza kutegua kitendawili husika kwa sababu ni kitendawili kinachotumika katika jamii nyingi. Aidha, wanafunzi hao waliweza kuhusisha dhana ya nyumba kutokuwa na mlango na umbo la yai ambalo halina uwazi wowote lakini kifaranga huishi humo hadi kinapoanguliwa. Kielelezo 2.3.19 ni jibu la mwanafunzi aliyetegua kitendawili.

**Kielelezo 2.3.19**


20. "Nyumba yangu haina mlango." Jibu la kitendawili hiki ni lipi? yai

Kielelezo 2.3.19 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyetegua kitendawili.

Aidha, wanafunzi 199,492 (asilimia 20.3) walipata alama 0 kwani waliandika maneno ambayo hayategui kitendawili husika. Wanafunzi hao hawakuwa na uelewa wa kitendawili hicho japokuwa ni miongoni mwa vitendawili vinavyotumika sana

katika jamii hasa kwa rika la watoto. Wanafunzi hao waliandika maneno kama vile *kulipa*, *rushwa* na *tausi* kama ilivyooneshwa kwenye kielelezo 2.3.20 cha jibu la mmoja wa wanafunzi aliyeshindwa kubaini neno linaloweza kutegua kitendawili alichoulizwa.

**Kielelezo 2.3.20**

20. "Nyumba yangu haina mlango." Jibu la kitendawili hiki ni lipi? kulipa

Kielelezo 2.3.20 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika neno ambalo halitegui kitendawili husika.

## 2.4 Sehemu D: Ufahamu

Sehemu hii ililenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika kusoma na kujibu maswali kutokana na kifungu cha habari alichokisoma. Wanafunzi walipewa kifungu cha habari kifuatacho:

*Mzee Magali anaishi katika kijiji cha Mailisita. Mke wa mzee Magali anaitwa Roza, ni mwanamke mkarimu sana. Familia hiyo hujishughulisha na kilimo cha mboga na matunda. Kila mwaka mzee Magali huvuna mboga nyingi sana pamoja na matunda. Siku ya Ijumaa hupeleka sokoni mchicha, nyanya, biringani, bamia na nyanya chungu. Aidha, siku ya Jumamosi hupeleka pia parachichi, maembe, matango na machungwa.*

*Mzee Magali anawasomesha watoto wake kwa kutumia pesa anazopata kutokana na kuuza mazao. Kutokana na faida aliyoipata mwaka jana alinunua trekta na mashine ya*

*kusaga. Trekta hiyo inamsaidia katika kilimo. Pia humpatia pesa kwa kuwa hutumia kuwalimia wanakijiji wenzake.*


**Swali la 21:** Mzee Magali anaishi katika kijiji gani? __________.

**Jedwali 2.4.1:** Idadi na Asilimia ya Wanafunzi katika kila Alama

| Alama | 0 | 2 |
|---|---|---|
| **Idadi ya Wanafunzi** | 758,314 | 222,675 |
| **Asilimia ya Wanafunzi** | 77.3 | 22.7 |

Swali lilimtaka mwanafunzi kusoma kifungu cha habari, kuelewa na kisha kutaja mahali anapoishi Mzee Magali. Jedwali 2.4.1 linaonesha kuwa ufaulu ulikuwa mzuri kwani wanafunzi 758,314 (asilimia 77.3) walijibu swali hili vizuri kwa kuandika jibu sahihi "Mailisita." Wanafunzi hao waliweza kurejea mawazo yaliyopo katika aya ya kwanza, mstari wa kwanza unaotaja jina la mahali anapoishi mzee Magali. Kielelezo 2.4.1 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu swali hili vizuri.

**Kielelezo 2.4.1**



21. Mzee Magali anaishi katika kijiji gani? Mailisita

Kielelezo 2.4.1 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kukumbuka jina la mahali anapoishi mzee Magali.

Aidha, wanafunzi 222,675 (asilimia 22.7) walishindwa kulijibu swali hili vizuri jambo linaloonesha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha katika kuhawilisha maudhui yaliyomo katika kifungu cha habari walichopewa. Katika kifungu

cha habari, mahali anapoishi mzee Magali pametajwa wazi katika aya ya kwanza, mstari wa kwanza. Miongoni mwa wanafunzi hao wapo walioandika majibu kama vile*, sigoli, baba*, *mzee Magali*, na *anaitwa Roza.* Kielelezo 2.4.2 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kuelewa alichokisoma na hivyo hakukumbuka jina la mahali anapoishi Mzee Magali.

**Kielelezo 2.4.2**


21. Mzee Magali anaishi katika kijiji gani? anaitwa Roza

Kielelezo 2.4.2 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyetaja jina la mke wa Mzee Magali badala ya mahali anapoishi Mzee Magali.

**Swali la 22:** Mke wa Mzee Magali anaitwa nani? ________________

**Jedwali 2.4.2:** Idadi na Asilimia ya Wanafunzi katika kila Alama

| Alama | 0 | 2 |
|---|---|---|
| **Idadi ya Wanafunzi** | 758,689 | 222,300 |
| **Asilimia ya Wanafunzi** | 77.3 | 22.7 |

Swali lilimtaka mwanafunzi kutaja jina la mke wa Mzee Magali. Jedwali 2.4.2 linaonesha kuwa ufaulu ulikuwa mzuri kwani wanafunzi 758,689 (asilimia 77.3) walijibu swali hili vizuri kwa kuandika jibu “Roza”, ambalo ni jibu sahihi kama linavyojidhihirisha katika sentensi ya pili, ya aya kwanza. Kielelezo 2.4.3 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika jibu sahihi.

**Kielelezo 2.4.3**

22. Mke wa mzee Magali anaitwa nani? Roza

Kielelezo 2.4.3 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyebaini jina la mke wa Mzee Magali lililotajwa katika habari aliyoisoma**.**

Wanafunzi 222,300 (asilimia 22.7) waliandika majibu yasiyo sahihi jambo linaloonesha kuwa hata kama waliweza kusoma kifungu cha habari hawakuelewa maudhui ya habari hiyo. Hivyo kushindwa kutaja jina la mke wa Mzee Magali ambalo limeandikwa kwenye kifungu cha habari. Majibu ya wanafunzi hao yalikuwa kama vile *trekta*, *anawasomesha,* na *mkee.* Kielelezo 2.4.4 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika jibu ambalo siyo jina la mke wa mzee Magali.

**Kielelezo 2.4.4**

22. Mke wa mzee Magali anaitwa nani? mkee

Kielelezo 2.4.4 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi ambalo halikuwa na uhusiano na jina la mke wa Mzee Magali.


**Swali la 23:** Familia ya Mzee Magali hulima nini? ____________________

**Jedwali 2.4.3:** Idadi na Asilimia ya Wanafunzi katika kila Alama

| Alama | 0 | 1 | 2 |
|---|---|---|---|
| **Idadi ya Wanafunzi** | 313,391 | 64,746 | 602,604 |
| **Asilimia ya Wanafunzi** | 31.9 | 6.6 | 61.5 |

Swali lilimtaka mwanafunzi kutaja aina ya mazao ambayo familia ya mzee Magali hujishughulisha nayo. Jedwali 2.4.3 linaonesha kuwa ufaulu ulikuwa mzuri kwani wanafunzi 667,350 (asilimia 68.1) walipata kati ya alama 1 na 2. Miongoni mwao asilimia 61.5 waliandika "mboga na matunda" ambalo ndilo jibu sahihi na kupata alama zote 2." Aidha, asilimia 6.6 waliandika neno moja tu kati ya "mboga" au "matunda" hivyo walipata alama 1." Kielelezo 2.4.5 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika jibu sahihi.

**Kielelezo 2.4.5**


23. Familia ya Mzee Magali hulima nini? mboga na matunda

Kielelezo 2.4.5 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi waliyeandika kwa usahihi mazao yanayolimwa na familia ya Mzee Magali.


Wanafunzi 378,985 (asilimia 38.5) walishindwa kabisa kuandika jibu sahihi katika swali hili. Miongoni mwa majibu waliyoandika ni kama vile *trekta*, *faida* na *hujishughulisha na kulima*. Mwanafunzi aliyeandika jibu *trekt*a alihusisha neno hilo na nyenzo inayotumika katika kilimo badala ya kuandika aina ya mazao yanayolimwa na familia ya Mzee Magali. Aidha, mwanafunzi aliyeandika *hujishughulisha na kulima* alitaja shughuli ya kiuchumi inayofanywa na familia ya Mzee Magali badala ya aina ya mazao. Kielelezo 2.4.6 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kubaini maelekezo ya swali.

**Kielelezo 2.4.6**

23. Familia ya Mzee Magali hulima nini? trekta

Kielelezo 2.4.6 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika trekta kwa kuhusianisha zana inayotumika katika kilimo badala ya aina ya mazao yanayolimwa na familia ya Mzee Magali.

**Swali la 24:** Siku ya Jumamosi Mzee Magali hupeleka nini sokoni? ________________________




**Grafu 2.4.1:** Asilimia ya Wanafunzi katika kila Alama

Swali lilimtaka mwanafunzi kuandika vitu ambavyo Mzee Magali hupeleka sokoni siku ya Jumamosi. Grafu 2.4.1 inaonesha kuwa swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango cha wastani ambapo wanafunzi 564,763 (asilimia 57.5) walipata kati ya nusu alama na 2. Kwa mujibu wa kifungu cha habari vitu ambavyo Mzee Magali

hupeleka sokoni siku ya Jumamosi ni vinne ambavyo ni "Parachichi, maembe, matango na machungwa." Wanafunzi walioandika vitu vyote vinne kwa usahihi walikuwa asilimia 52.7 na walipata alama zote 2. Asilimia 1.2 walipata nusu alama kwa vile waliandika kitu kimoja tu. Asilimia 2.4 walipata alama 1 kwa vile waliandika vitu viwili tu na asilimia 1.2 walipata alama 1 na nusu kwa vile waliandika vitu vitatu tu. Kielelezo 2.4.7 ni jibu la mmoja wa wanafunzi aliyeandika vitu ambavyo Mzee Magali hupeleka sokoni siku ya Jumamosi.

**Kielelezo 2.4.7**


24. Siku ya Jumamosi mzee Magali hupeleka nini sokoni?

Parachichi, maembe, matango na machungwa

Kielelezo 2.4.7 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeorodhesha vitu ambavyo Mzee Magali hupeleka sokoni siku ya Jumamosi.

Wanafunzi 416,226 (asilimia 42.5)walishindwa kutoa majibu sahihi ya swali hili na hivyo kupata alama 0. Baadhi ya wanafunzi hao waliandika vitu ambavyo Mzee Magali hupeleka sokoni siku ya Ijumaa badala ya Jumamosi na wengine walinakili maneno ambayo ni sehemu ya swali badala ya kulijibu. Kielelezo 2.4.8 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika vitu alivyopeleka Mzee Magali sokoni siku ya Ijumaa badala ya Jumamosi kama alivyooulizwa katika swali.


**Kielelezo 2.14**




Kielelezo 2.4.8 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika mchicha ambao hupelekwa sokoni Ijumaa badala ya Jumamosi. Mwanafunzi huyu alishindwa kuweka nafasi kati ya neno na neno jambo linaloonesha hakuwa na umahiri wa stadi ya kuandika.

**Swali la 25:** Mwaka jana Mzee Magali alinunua vitu gani?__________________

**Chati 2.4.1:** Asilimia ya Wanafunzi katika kila Alama




Swali lilimtaka mwanafunzi kutaja vitu ambavyo Mzee Magali alinunua mwaka jana. Chati 2.4.1 inaonesha kuwa swali hili lilijibiwa kwa kiwango kizuri kwani wanafunzi 669,583 (asilimia 68.3) walipata kati ya alama 1 au 2. Miongoni mwao asilimia 57.6 waliandika "Trekta na mashine ya kusaga" ambalo ndilo jibu sahihi na kupata alama zote 2." Aidha, asilimia 10.7 walijibu kwa kuandika "trekta" au "mashine ya kusaga" hivyo

walipata alama 1. Kielelezo 2.4.9 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika jibu kwa usahihi.

**Kielelezo 2.4.9**

25. Mwaka jana mzee magali alinunua vitu gani? trekta na mashine ya kusaga

Kielelezo 2.4.9 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika kwa usahihi vitu alivyonunua Mzee Magali mwaka jana.

Wanafunzi 311,406 (asilimia 31.7) walipata alama 0. Wanafunzi hao hawakuweza kufahamu vitu ambavyo Mzee Magali alinunua mwaka jana. Kielelezo 2.4.10 ni jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kubaini vitu alivyonunua Mzee Magali mwaka jana, hivyo kuandika baadhi ya mazao anayolima yakiwemo matunda.

**Kielelezo 2.4.10**

25. Mwaka jana mzee magali alinunua vitu gani? matunda

Kielelezo 2.4.10 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika mazao badala ya bidhaa alizonunua Mzee Magali mwaka jana.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA MBALIMBALI

Upimaji wa Kiswahili ulihususha mada nne ambazo ni *Kusoma kwa Utambuzi na Kuandika* (imla), *Sarufi na Matumizi ya Lugha, Lugha ya Kifasihi, na Ufahamu*. Uchambuzi unaonesha kuwa maswali yaliyojibiwa vizuri ni swali la 1, 2, 3, 4 na 5 kutoka mada ya *Kusoma kwa Utambuzi na Kuandika* (Imla) ambayo yalikuwa na ufaulu wa asilimia 89.9, 88.8, 89.5, 85.2 na 82.8 ya wanafunzi, mtawalia. Aidha, swali la 9 kutoka mada ya *Sarufi na Matumizi ya Lugha* nalo lilijibiwa

vizuri na asilimia 80.9 ya wanafunzi. Maswali yaliyojibiwa vibaya ni swali la 14 kutoka mada ya *Lugha ya Kifasihi* ambapo ni asilimia 10.5 tu ya wanafunzi waliweza kuandika jibu sahihi. Swali hili lilijibiwa vibaya kuliko maswali mengine yote katika upimaji huu. Swali la 12 kutoka mada ya *Lugha ya Kifasihi* nalo lilikuwa na asilimia ndogo (14.7%) ya wanafunzi waliojibu kwa usahihi. Vilevile, maswali ya 8 na 15 yaliyotoka katika mada ya *Sarufi na Lugha ya Kifasihi* mtawalia, yalikuwa na ufaulu mdogo Swali la 8 ni asilimia 31.4 ya wanafunzi ndio waliochagua jibu sahihi. Swali la 15 ni asilimia 38.3 tu ya wanafunzi ndio walijibu swali hilo kwa usahihi. Uchambuzi wa ufaulu ulibaini kuwa mada ya *Kusoma kwa Utambuzi na Kuandika* (Imla) ndio yenye asilimia kubwa ya ufaulu katika maswali yote matano. Uchambuzi wa ufaulu wa wanafunzi kwa kila mada katika somo la Kiswahili umewasilishwa katika **kiambatisho**.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa namna wanafunzi walivyojibu maswali unaonesha kuwa kulikuwa na changamoto mbalimbali zilizowakumba wanafunzi wakati wakifanya maswali ya upimaji. Kwa ujumla, ufaulu wa wanafunzi ulikuwa mzuri kwa mada tatu na wa wastani kwa mada moja.

Japokuwa kumekuwa na ufaulu wa kiwango kizuri katika kila mada, bado juhudi zaidi zinahitajika katika ujifunzaji na ufundishaji wa mada zote ili umahiri wa wanafunzi katika stadi za Kusoma na Kuandika uimarike zaidi. Kupitia wadau mbalimbali wa lugha ya Kiswahili, somo hili linatakiwa kupewa kipaumbele kwa kuwawezesha wanafunzi kupata maarifa ya kutosha ili waweze kukabiliana na changamoto mbalimbali za kitaaluma na za kimaisha zinazohusiana na lugha ya Kiswahili.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Itambulike wazi kuwa Kiswahili ni lugha ya Taifa, ni sehemu ya utamaduni wa Mtanzania, na ni lugha inayoziunganisha nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na pia hutumika kimataifa. Hivyo, ni vyema juhudi endelevu za kuinua lugha hii zifanyike kuanzia shule za msingi hadi elimu ya juu. Kwa kufanya hivyo, lugha ya Kiswahili itakuwa imetendewa haki na kupewa hadhi inayostahili katika taifa hili.

Ili kuwawezesha wanafunzi kupata maarifa na ujuzi wa kutosha na kuboresha matokeo yao katika upimaji wa somo la Kiswahili, mambo yafuatayo hayana budi kuzingatiwa:

(a) Mamlaka husika zihakikishe kuwa shule zote za msingi zina vitabu vya kiada na ziada vya kutosha kwa ajili ya somo la Kiswahili ili wanafunzi waweze kumudu stadi ya kusoma. Aidha, kwa kutumia vitabu hivyo walimu watoe mazoezi mbalimbali ya kusoma kimya huku wakitumia mbinu mbalimbali za ufundishaji. Hii itawajengea wanafunzi uwezo wa kufanya uchambuzi ulio makini na kujenga mawazo kutokana na habari walizosoma hatimaye kumudu vyema mada ya ufahamu.

(b) Walimu wanaofundisha somo la Kiswahili katika shule za msingi wanatakiwa kufundisha mada zote kwa ukamilifu kama ilivyoelekezwa katika muhtasari. Mada ya Lugha ya Kifasihi itiliwe mkazo zaidi katika ufundishaji na ujifunzaji ili kuwawezesha wanafunzi kumudu matumizi ya methali, nahau na pia kutegua vitendawilli kwa usahihi.

(c) Ili kupata ujifunzaji na ufundishaji wenye mafanikio, walimu wanatakiwa kutoa mazoezi ya kutosha kwa wanafunzi yatakayowawezesha kumudu stadi ya kuandika. Mazoezi ya imla yawe ya kutosha ili kuwajengea wanafunzi uwezo wa kusikiliza na kuandika. Mrejesho wa matokeo ya mazoezi hayo utolewe kwa wanafunzi ili waweze kurekebisha dosari za uandishi. Dosari hizo ni pamoja na athari za lugha mama, kutomudu uandishi wa silabi mwambatano, kutomudu uandishi wa maneno ya mwambatano na kutoacha nafasi kati ya neno na neno.

(d) Wanafunzi wahamasishwe kutumia Kiswahili sanifu katika mazungumzo na maandishi yao ya kila siku ili kuboresha msamiati na sarufi ya lugha ya Kiswahili kwa ujumla.

**KIAMBATISHO CHA PEKEE**

## MUHTASARI WA UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA SOMO LA KISWAHILI KWA KILA MADA

| Na | Mada | UPIMAJI WA 2015 | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya Swali | % ya ufaulu | | |
| 1. | Kusoma kwa Utambuzi na Kuandika (Imla) | 1 | 89.9 | 87.24 | Vizuri |
| | | 2 | 88.8 | | |
| | | 3 | 89.5 | | |
| | | 4 | 85.2 | | |
| | | 5 | 82.8 | | |
| 2. | Ufahamu | 21 | 77.3 | 69.86 | Vizuri |
| | | 22 | 77.4 | | |
| | | 23 | 68.7 | | |
| | | 24 | 57.6 | | |
| | | 25 | 68.3 | | |
| 3. | Sarufi na Matumizi ya Lugha | 6 | 79.2 | 65.42 | Vizuri |
| | | 7 | 55.8 | | |
| | | 8 | 31.4 | | |
| | | 9 | 80.9 | | |
| | | 10 | 67.7 | | |
| 4. | Lugha ya Kifasihi | 11 | 66.8 | 54.48 | Wastani |
| | | 12 | 14.7 | | |
| | | 13 | 65.5 | | |
| | | 14 | 10.5 | | |
| | | 15 | 38.3 | | |
| | | 16 | 68.9 | | |
| | | 17 | 79.4 | | |
| | | 18 | 50.3 | | |
| | | 19 | 70.7 | | |
| | | 20 | 79.7 | | |